# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1016

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi Elimu ya Amali

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-817-0

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi Elimu ya Amali nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA MISINGI YA UKUFUNZI WA KARAKANA/MAABARA
# MAFUNZO YA ASTASHAHADA YA UKUFUNZI WA KARAKANA/MAABARA
# ELIMU YA AMALI
# 2023

© Taasisi ya ElimuTanzania, 2023

Chapa ya Kwanza, 2023

ISBN 978-9987-09-817-0

Taasisi ya ElimuTanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam, Tanzania.

Simu: +255 735 041 168 / +255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.(2023). *Muhtasari wa Somo la Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Elimu ya Amali*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri Muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

**Yaliyomo**

Orodha ya Majedwali ........ iv
Vifupisho ........ v
Shukurani ........ vi

1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ........ 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 2
  3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu ........ 2
  3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu ........ 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara (Elimu ya Amali) ........ 3
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mkufunzi Tarajali wa Karakana/Maabara na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4
  6.1 Mkufunzi ........ 4
  6.2 Mkufunzi Tarajali wa Karakana/Maabara ........ 5
  6.3 Mzazi/Mlezi ........ 5
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6
9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6
10.0 Idadi ya Vipindi ........ 7
11.0 Maudhui ya Somo ........ 7

Bibliografia ........ 11

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu ........ 7

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Somo ........ 8

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

## Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Somo la Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Elimu ya Amali wa mwaka 2023 yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za umma na zisizo za umma. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya kusimamia kazi ya maboresho ya mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu na ukufunzi iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la maboresho ya Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara ni la lazima kwa wakufunzi tarajali wote wa Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Elimu ya Amali. Somo hili linalenga kukuza uwezo wa mkufunzi tarajali wa karakana/maabara katika kutumia misingi ya ukufunzi wa karakana/maabara kwa kuzingatia maadili na nadharia za ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo. Aidha, somo hili litamwezesha mkufunzi tarajali kuwa na weledi na umahiri wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa fani ya Elimu ya Amali. Vilevile, ataweza kumudu umahiri uliokusudiwa na kuwajibika vyema kwa wanafunzi na kwa taifa kwa ujumla.

Muhtasari umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara katika Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Elimu ya Amali. Muhtasari huu unatafsiri umahiri uliobainishwa kwenye Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Elimu ya Amali wa Mwaka 2023. Muhtasari unatoa maelekezo ya kumwezesha mkufunzi kuandaa mchakato wa ufundishaji kwa ufanisi. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi kwa mkufunzi kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara zitakazokuza stadi za amali na stadi za karne ya 21 zikiwemo ubunifu, mawasiliano, ushirikiano, fikra tunduizi na utatuzi wa changamoto.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba ili kuweza kujithamini na kujiamini;
(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;
(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwezesha mkufunzi tarajali wa karakana/maabara:
(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;
(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;
(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kukuza utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na
(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (*classroom-based action research*).

**4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Elimu ya Amali**

Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi wa Elimu ya Amali yanalenga kumwezesha mkufunzi tarajali wa karakana/maabara:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji kwa vitendo wa fani za elimu ya amali;
(b) Kumudu mbinu za kufundisha kwa vitendo fani za elimu ya amali;
(c) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalum ya ujifunzaji kwa vitendo na kutoa afua stahiki; na
(d) Kumudu misingi ya usimamizi wa karakana/maabara.

**5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi**

Muhtasari huu umejumuisha umahiri mkuu na umahiri mahususi ambao unatarajiwa kujengwa kwa mkufunzi tarajali wa karakana/maabara Elimu ya Amali kama unavyoainishwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya ukufunzi wa Elimu ya Amali | 1. 1 Kumudu maadili ya ukufunzi |
| | 1. 2 Kumudu mbinu na kanuni za ujifunzaji wa Elimu ya Amali |
| 2.0 Kumudu Mtaala wa Elimu ya Amali | 2.1 Kumudu maandalizi ya somo la vitendo |
| 3.0 Kumudu misingi ya kuwezesha mwanafunzi kujifunza katika mazingira jumuishi | 3.1 Kumudu mbinu za kuboresha ujifunzaji na ufundishaji wa Elimu ya Amali katika mazingira jumuishi |
| 4.0 Kumudu misingi ya upimaji na tathmini katika elimu ya amali | 4.1 Kumudu mbinu za upimaji kwa vitendo katika Elimu ya Amali |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mkufunzi Tarajali wa Karakana/Maabara na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji hutegemea ushirikiano baina ya mkufunzi, mkufunzi tarajali wa karakana/maabara na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatavyo:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kumwezesha mkufunzi tarajali wa karakana/maabara kujenga umahiri uliokusudiwa;
(c) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia;
(d) Kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;
(e) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mkufunzi tarajali wa karakana/maabara bila kujali tofauti zao;
(f) Kumlinda mkufunzi tarajali wa karakana/maabara awapo chuoni;
(g) Kufundisha na kujifunza pamoja na mkufunzi tarajali wa karakana/maabara;
(h) Kufuatilia maendeleo ya kila siku ya mkufunzi tarajali wa karakana/maabara;
(i) Kubaini mahitaji ya mkufunzi tarajali wa karakana/maabara na kumpatia afua stahiki;
(j) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika maendeleo ya ujifunzaji wa mkufunzi tarajali wa karakana/maabara; na
(k) Kuwezesha uchopekaji wa masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na
(l) Ujifunzaji.

**6.2 Mkufunzi Tarajali wa Karakana/Maabara**

(a) Mkufunzi tarajali wa karakana/maabara anatarajiwa:
(b) Kushiriki katika shughuli zote za ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo;
(c) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na
(d) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

**6.3 Mzazi/Mlezi**

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mkufunzi tarajali wa karakana/ maabara katika ujifunzaji;
(b) Kufuatilia mwenendo wa kitabia na maadili ya mkufunzi tarajali wa karakana/ maabara;
(c) Kuhakikisha ulinzi na usalama wa mkufunzi tarajali wa karakana/ maabara;
(d) Kumpatia mkufunzi tarajali wa karakana/ maabara vifaa vinavyotumika katika shughuli ya ujifunzaji; na
(e) Kuhakikisha mkufunzi tarajali wa karakana/ maabara anapata mahitaji muhimu.

**7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

Muhtasari huu unasisitiza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kumwezesha mkufunzi tarajali wa karakana/maabara kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu shirikishi kumwezesha mkufunzi tarajali wa karakana/maabara kujifunza kwa kuzingatia mahitaji anuai na uwezo wake. Mbinu hizo ni pamoja na zile zinazomwezesha mkufunzi tarajali wa karakana/maabara kufikiri, kutumia teknolojia kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali na kushiriki katika kutoa mrejesho. Njia nyingine ni ziara za kimasomo, majadiliano katika vikundi, kazi za vitendo, kazimradi, utafiti, majaribio ya kisayansi na nyingine kulingana na muktadha wa fani ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Amali zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji na uwezo wa mkufunzi tarajali wa karakana/ maabara. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha kuwa mkufunzi tarajali wa karakana/maabara anapata nafasi ya kujifunza kuandaa na kutumia zana mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji. Zana hizo zimependekezwa katika Jedwali Na. 3 katika kipengele cha zana.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji wa kila siku wa mkufunzi tarajali wa karakana/maabara na mitihani ya mwisho ya kukamilisha ngazi husika. Upimaji wa ndani utaratibiwa chuoni wakati wa ufundishaji na ujifunzaji na upimaji wa nje utaratibiwa na mamlaka inayohusika.

Mbinu mbalimbali za upimaji zitatutamika kupima nadharia na vitendo katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu hizo ni pamoja na bungua bongo, majaribio, mazoezi, mitihani ya kati na mtihani wa mwisho kulingana na aina ya upimaji, mahitaji na umahiri unaokusudiwa kujengwa. Baadhi ya zana zinazotarajiwa kutumika katika upimaji na tathimini ni orodha hakiki, mkoba wa kazi na fomu za maendeleo ya ujifunzaji wa  mkufunzi tarajali wa karakana/maabara.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Upimaji endelevu utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji wa mwisho utachangia asilimia thelathini (30%). Aidha, mchanganuo wa alama za upimaji endelevu utakuwa kama ifuatavyo; Mtihani wa mwisho wa mwaka utachangia 10%, Kazimradi itachangia 15%, ufundishaji kiduchu utachangia 20% na Ufundishaji wa kipindi utachangia 25%. Msimamizi tarajali wa karakana anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia 50% na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafikisha 50%, msimamizi tarajali wa karakana anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Alama za upimaji zimeoneshwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Shughuli ya Upimaji | Mgawanyo wa Asilimia |
|---|---|
| Mtihani wa mwisho wa mwaka | 10% |
| Kazimradi | 15% |
| Ufundishaji kiduchu | 20% |
| Ufundishaji shule jirani | 25% |
| **Jumla** | **70%** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Misingi ya Ukufunzi wa Karakana/Maabara Mafunzo ya Astashahada ya Ukufunzi Elimu ya Amali unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji za mkufunzi tarajali wa karakana/maabara. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni kumi na tano (15) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Somo

Maudhui ya somo yamegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo ni: umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana/vifaa na idadi ya vipindi kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Somo*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya ukufunzi wa Elimu ya Amali | 1.1 Kumudu maadili ya ukufunzi | Kuchambua miongozo inayosimamia maadili katika ufundishaji na ujifunzaji | Dhana za maadili na nidhamu katika ujifunzaji zimechambuliwa kwa kuzingatia tofauti kati ya maadili na nidhamu, miongozo inayosimamia maadili katika ujifunzaji, tabia na mienendo ya wanafunzi darasani, mbinu za kudhibiti nidhamu kwa wanafunzi, mbinu za kuboresha maadili katika ujifunzaji na ushauri kuhusu masuala ya maadili na nidhamu kwa wanafunzi | • Miongozo inayohusu maadili katika elimu | 104 |
| | 1.2 Kumudu mbinu na kanuni za ujifunzaji wa Elimu ya Amali | Kuchambua mbinu na kanuni za kufundisha kwa vitendo | Dhana ya mbinu na kanuni za ujifunzaji kwa vitendo zimechambuliwa kwa kuzingatia mbinu za ujifunzaji na kanuni za ufundishaji kwa vitendo | • Miongozo ya ufundishaji katika elimu ya amali<br>• Makala/majarida<br>• Ramani ya dhana *(concept map)*<br>• Video fupifupi kuhusu mbinu na kanuni za kufundisha kwa vitendo | 110 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu Mtaala wa Elimu ya Amali | 2.1 Kumudu maandalizi ya somo la vitendo | Kutafsiri katika vitendo andalio la somo la vitendo | Dhana ya andalio la somo kwa vitendo imechambuliwa kwa kuzingatia shughuli katika kila kipengele na mahitaji au vifaa vya kutekeleza somo kwa vitendo | • Andalio la somo<br>• Ramani ya dhana<br>• Matini za ufundishaji | 140 |
| 3.0 Kumudu misingi ya kuwezesha mwanafunzi kujifunza katika mazingira jumuishi | 3.1 Kumudu mbinu za kuboresha ujifunzaji na ufundishaji wa Elimu ya Amali katika mazingira jumuishi | Kumudu mbinu za kufundisha kwa vitendo wanafunzi wenye mahitaji maalumu | Dhana ya uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika elimu jumuishi imechambuliwa kwa kuzingatia ubainishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika muktadha wa elimu kwa vitendo na uandaaji wa mpango binafsi wa ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi | • Miongozo ya utekelezaji wa elimu jumuishi<br>• Makala za elimu jumuishi katika muktadha wa elimu ya amali | 46 |
| 4.0 Kumudu misingi ya upimaji na tathmini katika elimu ya amali | 4.1 Kumudu mbinu za upimaji kwa vitendo katika elimu ya amali | (a) Kuchambua mbinu na zana za upimaji kwa vitendo katika Elimu ya Amali | Mbinu na zana za upimaji kwa vitendo zimechambuliwa kwa kuzingatia muktadha wa mafunzo kwa vitendo | • Video fupifupi za mbinu na upimaji kwa vitendo<br>• Matini za upimaji katika Elimu ya Amali | 60 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutumia zana za upimaji kwa vitendo | Upimaji kwa vitendo umefanyika kwa kutumia mbinu na zana za upimaji kwa vitendo katika muktadha wa elimu ya amali | • Zana za upimaji katika mafunzo ya amali | |

## Bibliografia


Alexander, P. A., & Winne, P. H. (2012). *Handbook of educational psychology*. Routledge.

Bond, T. (2015). Standards and ethics for counselling in action. *Standards and Ethics for Counselling in Action*, 1-352.

Boronski, T., & Hassan, N. (2020). *Sociology of education*. Sage.

Capuzzi, D., & Stauffer, M. D. (2016). *Counseling and psychotherapy: Theories and interventions*. John Wiley & Sons.

Davies, S., & Guppy, N. (2010). *The schooled society: An introduction to the sociology of education*. Oxford University Press.

Duchesne, S., & McMaugh, A. (2018). *Educational psychology for learning and teaching*. Cengage AU.

European Union. (2022). *Vocational education and training Skills for today and for the future*. Publications Office of the European Union

Government of Tanzania. (2016). *National Skills Development Strategy* 2016/17-2025/26. Ministry of Education, Science and Technology and Prime Minister's Office Labour, Youth Employment and Persons with Disabilities

Ministry of Education and Culture. (1997). *Syllabus for Diploma in Education*. Ministry of Education and Culture.

Ministry of Education, Science and Technology. (2019). *National Curriculum Framework for Basic and Teacher Education*. TIE.

Nevid, J. S. (2012). *Psychology: Concepts and applications*. Cengage Learning.

Nevid, J. S. (2021). *Essentials of psychology: Concepts and applications*. Cengage Learning.

Salkind, N. J. (Ed.). (2008). *Encyclopedia of educational psychology*. SAGE publications.

Slavin, R. E. (2014). Educational psychology: Theory and practice. Pearson Higher Ed. Teacher training in Norway.

Slavin, R. E., & Davis, N. (2006). *Educational psychology: Theory and practice*. Pearson

Tanzania Institute of Education. (2003). *Moduli ya Somo la Misingi ya Elimu: Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti.* Tanzania Institute of Education.

Tanzania Institute of Education. (2013). *Mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti elimu ya msingi: Moduli ya kujifunzia somo la ualimu.* Tanzania Institute of Education.

UNESCO (2015). *Technical and Vocational Education Strategy (2016- 2021)*. UNESCO

United Republic of Tanzania. (2008). *Education Sector Development Programme 2008-2017*. Mninistry of Education, Science and Technology.

United Republic of Tanzania.(2010). *National Strategy for Growth and Reduction of Poverty*. United Republic of Tanzania.